Tazama video: www.atomohivtest.com

Unahitaji vifaa hivi vinne:



SW **Ungependa kupata msaada zaidi? Geuza kurasa.**

1 **Nawa** na upanguse mikono. **Angalia tarehe ya mwisho** kabla ya kufungua kipochi.



2 **Kanda** ykidole chako kwa sekunde 5 hadi 10.



3 **Geuza kwa wororo** na **utoe** tabo ya kijani, kisha uitupe.



4 **Bofya** kitufe cha kijivu ili **udunge kidole.**

MUHIMU
Itadunga mara moja tu!

5 Weka jaribio juu ya maagizo kando ya matokeo.

6 **Bonyeza kwa nguvu** nyuma ya sehemu iliyodundwa ili upate damu.

7 **Jaza** damu ndani ya **tyubu ya damu**, ikiwa tyubu yadamu hai jazwi bonyeza kidole tena ili ujaze damu.



MUHIMU
Ukipata tatizo, futa kidole kisha ubonyeze tena



8 Shika jaribio juu ya meza. Sasa **geuza juu chini tyubu ya damu** kwenye chombo.



MUHIMU
Hakikisha damu imetoka kwenye tyubu na kuingia vizuri kwenye chombo

9 Ongeza **matone 4** kwenye chombo.



MUHIMU
Matone 4

10 Subiri **dakika 15** kabla ya kusoma matokeo. Usisubiri zaidi ya dakika 20.



Matokeo

Hakikisha unasubiri dakika 15.

Ikiwa kidole chako bado kinavuja damu tumia shashi.

Linganisha kwa uangalifu matokeo yako na mapendekezo ya rangi nyekundu, ya chungwa, au ya kijani.

Kwa habari zaidi kuhusu VVU, angalia ukurasa unaofuata.

Hasi kwa VVU

Ikiwa **mstari mmoja** unajitokeza kwenye C, wewe ni hasi kwa VVU. Hakupaswi kuwa na mstari kwenye T.

Hili ni jaribio la kwanza.

Jaribu tena baada ya **Miezi 3**.

Angalia kadi ya utunzaji kwa habari zaidi.



Jaribio halikufanya kazi

Ikiwa **hakuna mstari kwenye C**, jaribio halikufanya kazi.

Hili ni jaribio la kwanza.

Nenda kwenye kliniki ili uchunguzwe zaidi.

Angalia kadi ya utunzaji kwa habari zaidi.



Chanya kwa VVU

Mistari miwili ikijitokeza, hata ikiwa ni hafifu sana, wewe ni chanya kwa VVU.

Hili ni jaribio la kwanza.

Nenda kwenye kliniki ili uchunguzwe zaidi.

Angalia kadi ya utunzaji kwa habari zaidi.



MUHIMU
Acha jaribio hapa, hiyo inasaidia kujaza tyubu ya damu

ARST-0A-037 revEN3

atomo | KUJIPIMA VVU

Unahitaji Msaada wa Kupima?

Kuchukua Damu Kwa Ajili ya Uchunguzi

Je, Unashindwa Kuondoa Kitufe cha Kijani?

- Kwanza geuza tabo kwa 90°, kisha kokota.

Unaogopa Itakuumiza?

- Usiogope, utahisi ni kama mpira unachapa kidole chako.
- Hutaiona sindano ikikuchoma.

Unasukuma kitufe cha kijani lakini huoni damu?

Je, kitufe kimetoka nje? Jaribu tena, sukuma kwa nguvu.

Taarifa: Itachukua damu kwa ajili ya kupima mara moja tu!

Je, kitufe kimeingia ndani?
Minya kidole chako, ikiwa kidole bado hakitoi damu - acha, na uanze kupima tena.

Kujaza bomba la damu

Sijui sehemu ya kuingizia damu?

- Bomba la damu lina rangi ya majani makavu, angalia picha kwenye hatua ya 7.
- Usiweke damu kwenye tundu la rangi ya kijivu.
- Usiweke damu moja kwa moja kwenye kitundu.
- Jaza damu kwenye bomba, itaweka kiwango sahihi cha damu.
- Kugusa bomba hakubadili matokeo ya vipimo.

Damu haijai kwenye bomba?

- Ikiwa uchafu umeingia kwenye damu, kifute kidole na ukiminye tena ili damu itoke.
- Kielekeze kidole upande wa chini.
- Iguse damu taratibu na ncha ya bomba.
- Ikiwa damu iliyotoka haitoshi, kifute kidole, na kisha kiminye tena ili damu itoke.
- Ikiwa damu inayotoka haitoshi tena kujaza bomba kikamili, basi matokeo ya kipimo hayatakuwa sahihi. Acha, na uanze kupima upya.

Kukamilisha Hatua za Kupima

Vipi ikiwa damu haitapita kutoka katika bomba mpaka kwenye tundu?

- Hakikisha bomba limejaa kikamili.
- Hakikisha damu inasukumwa vizuri kutoka katika bomba mpaka kwenye tundu.
- Ikiwa damu aisukumwi kwenda kwenye tundu- acha, na uanze kupima upya.

Sina uhakika kuhusu jinsi ya kuongeza matone manne kutoka katika chupa?

- Matone manne yanapaswa kwenda kwenye tundu juu ya damu.
- Usitikise chupa.
- Elekeza mdomo wa chupa chini na kisha uminye.

Sina uhakika kuhusu jinsi ya kusoma matokeo?

- Hakikisha unasubiri kwa dakika 15. Usisubiri zaidi ya dakika 20.
- Mistari iliyo karibu na “T” na “C” itakuonyesha matokeo ya kipimo.
- Fungua ukurasa chini na utafute sanduku lenye rangi inayofanana na matokeo yako ya kipimo.
- Kwa maelezo zaidi kuhusu matokeo ya kipimo, soma sehemu inayofuata: “Kuhusu Matokeo Yako ya Kipimo.”

Angalia **Kadi ya Huduma** ambayo inatia ndani sanduku la maelezo ya ziada na mawasiliano kwa ajili ya huduma ya msaada iliyo karibu nawe.

Kuhusu Matokeo Yako ya Kipimo

Kuna aina mbili ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ambavyo huitwa VVU-1 na VVU-2. Ikiwa utakuwa umeathiriwa na mojawapo ya aina ya virusi hivyo, mfumo wa kinga ya mwili wako itaunda kingamwili dhidi ya aina hiyo ya virusi. Kujipima mwenye VVU kumeandaliwa kwa njia ambayo inagundua kingamwili na kuonyesha ikiwa umeathiriwa na aina mojawapo ya virusi hivyo. Kipimo hiki kinaweza kugundua kingamwili hizo katika damu ya mwanadamu na unaweza kukitumia kupima mara moja tu.

Kipimo kitatoa matokeo baada ya dakika 15. Ikiwa matokeo ya kipimo chako yanaonyesha kwamba una VVU, yanaweza kuthibitishwa kwa kutumia njia ya badala ya kupima inayofanywa na wataalamu wa huduma ya afya, kwa kuwa hii ni huduma ya kuangalia tu.

Kipindi cha maambukizo ya VVU mpaka kipimo kinapoweza kutoa matokeo sahihi ni kipi?

Inachukua majuma 6 hadi 12 baada ya kuingia kwa VVU kabla ya mwili wako kuunda kingamwili ambazo zinatumika katika kipimo cha kugundua ikiwa una VVU. Wakati huo unaitwa “kipindi cha maambukizo ya VVU mpaka kipimo kinapoweza kutoa matokeo sahihi”. Ikiwa utajipima VVU katika kipindi hicho (miezi mitatu ya kwanza baada ya kuambukizwa VVU), kabla mwili wako haujaunda kingamwili utapata matokeo yasiyo sahihi kwamba huna VVU. Ikiwa unaamini umeambukizwa VVU, unashauriwa kupima tena baada ya kipindi hicho ambacho matokeo ya kipimo huenda yasiwe sahihi na uzungumze na mtaalamu wa huduma za afya hasa ikiwa hutarajii kupata matokeo yanayoonyesha kwamba huna VVU.

Ni jambo gani limetokea ikiwa matokeo ya kipimo yanaonyesha SINA VVU?

Kwanza hakikisha kwamba miezi mitatu imepita tangu wakati unapohisi uliambukizwa VVU. Ikiwa miezi mitatu imepita, na umefuata hatua za kipimo vizuri, Hivyo inawezekana usiwe na VVU. Ikiwa ulipima kabla ya miezi mitatu kupita mara tu ulipogundua kwamba umeambukizwa, unahitaji kurudia tena kupima inafika miezi mitatu. Kumbuka hiki ni kipimo cha kuangalia tu, ikiwa huna uhakika, omba ushauri, angalia **Kadi ya Huduma.**
Jambo muhimu: Pima tena baada ya miezi mitatu.

Ni jambo gani limetokea ikiwa matokeo ya kipimo yanaonyesha NINA VVU?

Inawezekana kuisha ukiwa na VVU na sasa watu wanaweza kuishi na VVU kwa muda mrefu, wakiwa nguvu na maisha mazuri. Kipimo cha kujipima mwenyewe ni kipimo cha kuangalia tu na kipimo kuonyesha kwamba una VVU si uthibitisho wa kuwa na virusi hivyo.

Ikiwa kipimo kinaonyesha kwamba una VVU, unahitaji kupima tena afya yako katika kituo cha kutoa huduma za afya kilicho karibu nawe. Ukigundua mapema kwamba umeambukizwa, utaanza mapema matibabu kama imethibitishwa kwamba una VVU. Angalia **Kadi ya Huduma** ambayo inatia ndani sanduku au tembelea tovuti www.atomotest.com kwa ajili ya kupata habari zaidi kuhusu jinsi ya kuendelea kupima.

Ni daktari au mtaalamu wa huduma za afya pekee anaweza kufanya tathimini na kukushauri kuhusu matibabu yanayokufaa. Ikiwa umepimwa na mtaalamu wa huduma za afya na kugundua kwamba una VVU, unaweza kuunganishwa katika huduma ya kupewa ushauri na, ikitegemea hali yako, unaweza kuwekwa katika mpango wa kupewa dawa za antiretroviral (ARV).

Ni jambo gani limetokea ikiwa kipimo changu hakifanyi kazi?

Inamaanisha kwamba hukupima kwa njia zinazofaa au kuna jambo ambalo ulikosea. Unahitaji kuanza kupima upya na kifaa kingine cha kupimia.

Ikiwa huna uhakika kama ulipima kwa njia inayofaa, nenda zahanati iliyo karibu au kwa mtaalamu wa huduma za afya ili upate msaada.

Nina wasiwasi kwamba inawezekana nimeambukizwa VVU siku chache zilizopita, ninapaswa kufanya nini?

Unapaswa kwenda kituo cha afya au kitengo cha Huduma za Dharura mapema iwezekanavyo, kabla ya saa 72, ambapo unaweza kupata huduma ya afya inayoitwa “PEP” (Post-Exposure Prophylaxis) itakayokulinda kutokana na VVU (Inawezekana huduma hii isipatikane kila nchi).

Kuhusu VVU

VVU ni nini?

VVU ni virusi vinavyosababisha upungufu wa kinga mwilini. Virusi hivi vinashambulia hasa mfumo wa kinga mwilini na baada ya muda vinadhoofisha uwezo wa mwili kupambana na magonjwa. VVU vinazaliana mwilini na kufanya isiwe rahisi kutibika, vinadhoofisha mfumo wa kinga mwilini na vinaweza kusababisha mwili upate ugonjwa Upungufu wa Kinga Mwilini (Ukimwi). Ingawa hakuna tiba kuondoa Ukimwi au VVU, lakini kupitia matibabu dawa yanaweza kuzuia usiwe ugonjwa sugu, na kuwa hali inayotishia uhai. Miaka ambazo mtu anaishi baada ya kugunduliwa kwamba ana VVU leo ni sawa na mtu asiye na VVU, ikiwa mtu huyo aliye na VVU atapata matibabu mapema na kutumia dawa kama alivyoagizwa.

Dalili za VVU ni zipi?

Njia moja tu ya kugundua kwamba una VVU ni kupima. Ni vizuri kupima ili kuepuka kuwaambukiza wengine bila kujua.

VVU inasambazwaje?

VVU inapatikana katika majimaji ya mwili kama vile kwenye damu, maziwa ya mama, shahawa, majimaji ya kwenye mkundu na majimaji ya kwenye uke. Maambukizi ya VVU yanaweza kutokea damu ya mtu mwenye VVU inapoingia kwenye mwili wa mtu asiye na VVU labda kupita kuwekewa damu ya mtu mwingine, kupitia shahawa, au majimaji ya mkundu au uke ya mtu mwenye VVU. Kuna uwezekano mkubwa sana kwa mtu mwenye magonjwa yanayopitishwa kingono kuambukizwa VVU, magonjwa hayo kama vile, chlamydia,kisonono, kaswende na magonjwa yanayobebwa na damu kama vile ugonjwa wa ini aina ya C. Mtoto mchanga anaweza kuambukizwa VVU kutoka kwa mama yake wakati wa kujifungua na wakati akinyonyeshwa hasa ikiwa ikiwa mama hakupata kinga mapema ya kuzuia maambukizi ya VVU kwa mtoto.

Matukio hatari ya kuambukizwa ni yapi?

“Matukio Hatari ya Kuambukizwa” ni mambo yote yanayoweza kuongeza nafasi ya kuambukizwa VVU, kama vile:

- Kufanya ngono isiyo salama na mtu mwenye VVU au ambaye hujui kama ana VVU.
- Kufanya ngono isiyo salama (ukeni au kwenye mkundu) na watu tofauti tofauti.
- Kutumia sindano moja na mtu ambaye ana VVU.

VVU haiwezi kuambukizwa kwa:

- Mambo kama vile (kushikana mikono, kutumia kikombe au nguo alizotumia mtu mwenye VVU, nk)
- Kumbusu
- Mate
- Jasho
- Machozi
- Hewa au maji hayawezi kuambukiza VVU

Maambukizo ya VVU yanaweza kuepukwa kwa:

- Kutumia kondomu unapofanya ngono.
- Kumwuliza mtu unayetaka kufanya naye ngono kuhusu historia yake ya matokeo ya vipimo vya VVU kujua ikiwa sasa hana VVU.
- Mtie moyo mwenzi wake mkapime VVU.
- Usitumie sindano iliyotumiwa na mtu mwingine.
- Tumia huduma ya Pre Exposure Prophylaxis (PrEP), huduma ya kumtibu mtu mwenye VVU, anayopewa mtu ambaye hana VVU ili kupunguza uwezekano wa kupata VVU. (Huduma hii inaweza isipatikane katika baadhi ya nchi)
- Kutumia huduma ya Post Exposure Prophylaxis (PEP), ambayo ikiwa itatumiwa kabla ya kupita saa 72 baada ya kuhisi umeambukizwa, inaaminika kwamba inapunguza uwezekano wa kupata VVU. (Huduma hii inaweza isipatikane katika baadhi ya nchi)

Tembelea www.atomohivtest.com ili utazame video za maelekezo. Ikiwa una swali lolote tuma barua pepe kwenda support@atomohivtest.com

atomo

Mhutasari wa Kipimo Virusi vya Ukimwi (VVU)

Kifaa cha kujipima mwenyewe kina kikaratasi ndani ya plastiki. Kipimo kinafanyika kwa kuweka tone la damu kwenye kikaratasi hicho cha kupimia na kusha kuweka matone ya kimiminika cha kupimia. Ukishapima, mistari miwili inaweza kutokea kwenye kikaratasi. Sehemu inayoonyesha matokeo itaonekana tu ikiwa kipimo kilifanywa kwa njia inayofaa. Mistari ya kipimo itaonekana tu ikiwa damu iliyowekwa ina kingamwili zinazozuia VVU

Matumizi Yaliyokusudiwa

Kifaa cha kujipima mwenyewe kinatumiwa mara moja tu, kinaonyesha rangi zinazoashiria kwamba mwili umetoa kingamwili, kipimo kinachogundua kingamwili Virusi vya Ukimwi Aina ya 1 (VVU-1) na Aina ya 2 (VVU-2) iliyopo kwenye damu. Jaribio la Kujipima HIV la Atomo limekusudiwa kutumiwa na watu ambao hawajazoezwa kama njia ya kujipima na kusaidia kutambua dalili za kuambukizwa VVU-1 na VVU-2 kutokana na damu nzima iliyotolewa moja kwa moja kupitia kukusanya damu kwa kutoka kwenye kidole. Kifaa kinahitaji damu kiasi 10ul. Matokeo ya jaribio yanaonyesha (“jaribio lako ni chanya” au “jaribio lako ni hasi”) na si ya kutumiwa na wakusanyaji wa damu.

ARST-0A-037 revEN3

Jaribio hili linatia ndani njia ya kudhibiti damu inayotolewa ili kuhakikisha kwamba jaribio linafanywa kwa usahihi; mstari huo wa kudhibiti unaonekana kwenye kifaa cha jaribio ikiwa mbinu sahihi inafuatwa.

Vifaa Vinavyotiwa Ndani

1 - Maagizo ya Utumiaji (IFU)
1 - Jaribio la Kujipima VVU la Atomo (pakiti iliyo na sehemu ya kutupia)
1 - Chupa ya Umajimaji wa Majaribio (Umajimaji)
1 - Karatasi ya kutupa takataka
1 - Kadi ya utunzaji

Vifaa ambavyo HAVIJATIWA ndani lakini vinahitajika

- Sanduku la shashi (au kitambaa kingine safi, kinachoweza kufyonza).
- Saa (kwa mfano ya mkononi, ya ukutani au simu ya mkononi) ili kupima muda unaposubiri matokeo.

Ilani za matumizi

- Haifai kwa kuwapimia watu wanaochanga damu
- Haifai kuwapimia watu walio na matatizo ya damu (k.m. walio na ugonjwa wa kuvuja damu)
- Haipaswi kutumiwa na watu wanaoogopa sindamo
- Haifai kutumiwa na watu ambao tayari ni chanya kwa VVU
- Haifai kutumiwa na watu wanaotumia dawa za kupunguza makali ya ugonjwa (ART)

Mapungufu ya Jaribio

- Huenda isitambue maambukizi ya VVU ambayo yametokea katika miezi 3 iliyopita.
- Mbinu hii, tahadhari, na tafsiri ya matokeo inapaswa kufuatwa unapotumia jaribio hili.
- Inaonyesha tu ikiwa kuna viini vinavyopatana na VVU.
- Haipaswi kutumiwa kuwa kipimo pekee cha kuambukizwa kwa VVU au matibabu yake.
- Matokeo chanya yanapaswa kuhakikishwa na mtaalamu wa afya. mtumiaji hapaswa kufanya uamuzi kuhusu afya kuhusu hali yake bila kwanza kuwasiliana na mtaalamu wa afya.
- Matokeo hayamaanishi kwamba kuna uwezekano wa kupatwa na VVU. ikiwa jaribio linaonyesha matokeo hasi na dalili za kiliniki zinaonekana, majaribio mengine kwa kutumia mbinu nyingine za kliniki zinapendekezwa.

Maonyo na Taadhari

- Kipimo kinafanya mara moja tu, usitumie kifaa kimoja kupima mara mbili.
- Matokeo yote kwamba una VVU yanapaswa kuthibitishwa kwa njia nyingine mbadala.
- Usitumie kifaa kilichopita wakati wake.
- Usitumie kifaa ikiwa kifurushi cha pakiti kimeharibika (k.m kupasuka, kina shimo au kibanio kimevunjwa) au kufunguliwa.
- Usitumie ikiwa sehemu ya dawa imeharibika au imelegea.
- Usitumie kimiminika kingine kwa ajili ya kipimo zaidi ya kile kilichotiwa ndani ya pakiti ya majaribio.
- Usitumie chupa yenye umajimaji wa majaribio ikiwa imefunguliwa au inavuja.
- Usiweke kimiminika hicho jichoni au kwenye ngozi.
- Ikiwa kimiminika kitawekwa kwenye kipimo bila kuwepo damu kwenye kifaa hicho, kipimo kitakuwa kimeharibika.
- Ikiwa maagizo hayatafuatwa kwa makini, unaweza kupata matokeo yasiyo sahihi.

Kutupa kifaa kilichotumika

Weka kifaa cha kupimia pamoja na vitu vyake vyote kutia ndani makasha yake ya kukibebea kwenye mkoba kuwekea uchafu unapewa. Kisha unaweza kufunga vizuri na kukitupa pamoja na takataka kutoka nyumbani.

Kuhifadhi

- Hifadhi kipimo kwenye eneo lenye nyuzi joto kati ya 2°C hadi 30°C
- Usihifadhi kwenye eneo lenye mwangaza wa jua
- Usifungue kifaa cha kupimia kama haupo tayari kupima. Tumi mara moja kifaa cha kujipima katika eneo lenye joto la kawaida.



Kupima

Uchunguzi wa Maabara

- Kwenye uchunguzi uliofanywa kwa wagonjwa 1000 kwa kutumia German Red Cross (Baden-Wuerttemberg-Hessen, Germany), vipimo vilivyofanywa kwa ukamili vilikuwa 100.0%.
- Kwenye uchunguzi uliofanywa kwa wagonjwa 320 kwa kutumia Institute of tropical Medicine (Antwerp, Belgium), vipimo vilivyofanywa kwa ubora vilikuwa 99.6% kwa ajili ya VVU-1 na 100.0% kwa ajili ya VVU-2.

Uchunguzi Nje ya Maabara

- Kwenye uchunguzi uliofanywa kwa wagonjwa 203 kwa kutumia the Kenya Medical Research Institute (Nairobi, Kenya), vipimo vilivyofanywa kwa ukamili vilikuwa 100.0%.

Watayarishaji

Atomo Diagnostics Pty. Ltd.
Level 2,
701-703 Parramatta Rd.
Leichhardt, NSW
2040 Australia
atomodiagnostics.com